Jarida la
UQAB
Toleo44 - Muharram 1442 H / Septemba 2020 M

# KUFAHAMU KWA KINA MAPINDUZI YA MALI



uqab.or.ke
uqab_htk
UQAB-Magazine-1911964012162253



////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////

# KUFAHAMU KWA KINA MAPINDUZI YA MALI

Mnamo ijumanne tarehe 18 Agosti, 2020, vyombo vyote vya habari viliangazia mapinduzi ya kijeshi nchini Mali huku vikitangazwa ya kwamba raisi Ibrahim Boubacar Keita ameondolewa madarakani kufuatia maandamano dhidi ya ufisadi, kudorora kwa uchumi na kudorora kwa hali ya usalama wa ndani ya nchi. Maonyesho ya watu wakisherehekea ushindi wa jeshi yalipeperushwa kote ulimwenguni hali hii ikiashiria ya kwamaba watu wanaunga mkono kubanduliwa kwa raisi mtawala licha ya nchi jumla ulimwenguni kutokubali mapindizu hayo.”Nina furaha kupindukia, tumeshinda tumekuja hapa kushukuru watu wote wa Mali kwasababau ni ushindi wa watu.” asema Mariam Cissé ambaye ni mfuasi wa upinzani aliekuwa akiiambia shirika la utangazi la AFP. "IBK ameshindwa na uwongozi, "alisema mwanajeshi mstaafu Ousmane Diallo, ambae alitumia majina maarufu ya rais alipokuwa akimtaja.”Watu ni washindi."

Mali ni nchi ya nane kwa ukubwa barani Afrika ikiwa na idadi ya watu million 19.1. Ina pakana nana nchi saba na ndio nchi ya tatu barani Afrika inayoongoza katika uzalishaji wa dhahabu pamoja na chumvi.  Madini mengine ambayo yana vunwa nchini Mali ni

kama vile Kaolite na mawe ya laimstoni.Nchi ya Mali ina kadiriwa kuwa na kiwango ziada cha  ya tani 17,400 za madini ya ureniam. Mnamo nyakati za kinyanganyiro kwa nchi za bara Afrika, Mali ilivamiwa na Ufaransa na mnamo kipindi cha mwaka wa 1905 jumla ya ardhi yake yote ilikuwepo chini ya usimamizi wa Ufaransa.  Mnamo tarehe 22 Septemba, 1960 wabepari wa kifaransa waliwapa wananchi wa Mali uhuru wao ingawaje bado nchi hio ilibakia chini ya athari zao kwa kupitia njia zakiujanja. Mnamo mwaka wa1963, nchi ya Mali ilifungamanishwa  na serikali ya Kifaransa kwa kupitia makubaliano ya BCEAO. Isitoshe utumizi wa sarafu ya CFA Zoni ya Franco kwa nchi ya Mali ilizidisha kupelekea Mali kuwa chini ya ushawishi wa mkoloni mambo leo Ufarasa licha ya kupata uhuru.



Tangu muungano wa Sovieti na taifa la Marekani  kubandua dola za Uindereza na Ufarasa kama Madola ma kuu ulimwenguni, Marekanai imekuwa ikiitazama  nchi za Afrika kaskazini na zile za jangwa la Sahara  kuwa ni sehemu za kushindaniwa  kwa unyakuzi wa mali ghafi kutoka kwa mabepari asli. Mwakani 2002, Marekani iliimarisha mahusiani yake na serikali ya Mali hii ikiwa ni kwa malengo ya kupiku ushawishi wa Ufaransa juu ya nchi ya Mali. Hivyo basi tangu siku hio, serikali za kibebaru za kimagharibi zimekuwa zikishindana kwa madhumuni ya kumiliki ushawishi dhidi ya serikali ya Mali na mwishowe kuipora malighafi zake.

Mnamo mapinduzi ya tarehe 22 Machi, 2012 yaliofanywa na Capteni Ahmadou Haya Sanogo, nchi ya ufaransa na Uingereza zilijitokeza kupinga mapinduzi hayo ya kijeshi ilhali Marekani haikukemea mapinduzi hayo bali iliomba watu wasitize kushambuliana na kukaa kwa amani. Ufaransa ilichukua hatua yakusimamisha msaada wake wa Kisiasa, uchumi na hata kijeshi pamoja ilhali Marekanai iliendelea kuisaidia nchi ya Mali kwa Dolari milioni137 kwa mwaka. Kwa kuwa kiongozi wa mapinduzi Kapteni Amadou (Ahmadou) Haya Sanogo aliwahi kuchaguliwa kutoka kikosi maalumu  cha Mali na balozi ya Marekani nchini Mali ili kuenda kufunzwa mafunzo ya mapambano dhidi ya ugaidi hivyo  mapinduzi-ilikuwa siajabumapenduzi hayo kuungwa mkono na Marekani hivyo basi kuashiria ushawishi  wa Ufaransa  nchini  Mali

umedorora na hata kubenduliwa na Marekani.


Mvutano sawia na huo baina ya Marekani na Ufarasa juu ya nchi ya Mali uliwahi kuonekana katika miezi ya hivi karibuni. Mwanzoni mwa mwaka huu, Baraza la Umoja wa Mataifa la Kiusalama liliamua ya kwamba Kikosi cha Umoja wa Mataifa cha takriban wanajeshi elfu kumi na wawili watatumwa nchini Mali kuanzia July- ambacho kitakuwepo ndani yao kikosi cha kijeshi cha nchi tofauti tofauti za Africa. Nyakati maafisa wa Marekani walikuwa wapigia debe  mabalozi wa nchi tofautu tofauti wa waunge mkono kwa kumchagua mmarekani bwana David Gressly, kama msimamizi maalum wa Umoja Mataifa nchini Mali ,Ufarasa ambayo ina dhamini kikosi cha kupambana na wanaodaiwa ni magaidi cha wanajeshi 4,5oo  maeneo ya Magharibi mwa Afrika sehemu za Sahel- nayo ilikuwa hairidhishi na uwepo wa usimamizi wa uwongozi wa Marekani bali kupendelea nafasi ya uwongozi wa kikosi cha Umoja wa Kimataifa cha kijeshi isimamiwe na mmoja kutoka nchi zinazo ongea lugha ya kifaransa -hali iliosababisha mzozo wa kidiplomasia baina ya Ufaransa na Marekana.

Ama kuhusiana na mapendezu ya kijeshi yaliotokea hii mwezi huu wa Agosti, kwakua wasimamizi wa mapenduzi wakijeshi waliwahi kuwa tena ni miongoni mwa wale waliopata mafunzo kutoka nchi ya Marekani, kuna uwezekano mkubwa tena kuwa waliofayanya mapenduzi wanazo baraka za Marekani hivyo basi kutumiwa kubandua ushawishi wa Ufaransa Serikalini Mali. Ni jambo la kusubiriwa vipi Ufaransa itajaribu kuregesha athari na ushawishi kwa serikali nchini Mali.

Ama kuhusu uwepo wa kutokea mara kwa mara mapenduzi ya kijeshi nchini Mali, hii huwa ni ishara tosha inayo ashiria kufeli kwa nidhamu tawala ya kidemokrasia. Maadamu nchi ya Mali itabaki masikini, na raia wake hawaiamini nidhamu tawala ya kidemorasia kwa kuwa inataasisi hafifu ambazo hazina fremu  bora zinazo hakikisha hakuna mmoja wapo anaweza pata mmamlaka yote kamili yasioweza kuhisabiwa-basi nchi ya Mali itazidi na kuendelea kuwa na Mapinduzi juu ya mapinduzi yanayo tokana na uingilio kati nanchi za nje za kikoloni. .

ABU LEILA 2020


LE MALI EST UN PAYS SOUVERAIN
SOUTIEN TOTAL A NOS FAMA
VIVE MALI
VIVE LE MALI Abba LA CDAO




//////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////

# UDHALIMU WA KIDEMOKRASIA KATIKA UGAVI WA MAPATO


Pendekezo juu ya ugawanyaji wa mapato baina ya kaunti ambalo litayapa mapendeleo makubwa maeneo yaliyo na idadi kubwa ya watu limesababisha mgawanyiko mkubwa katika bunge la Seneti. Kushindwa kwa Seneti kukubaliana juu ya msingi wa tatu wa mbinu ya ugawanyaji mapato natija yake imezitumbukiza kaunti katika kina zaidi cha mgogoro wa kifedha kwani sasa itachukua muda mrefu zaidi kwa kaunti kugawanya Sh316.5 bilioni zilizotengewa kama mapato ya ugavi adilifu katika mwaka wa fedha wa 2020/21. [Daily Nation]

Kikatiba, ugavi wa mapato ni kazi ya Tume ya Ugavi wa Mapato (CRA) ambayo ni kutoa mapendekezo kuhusiana na msingi wa ugavi adilifu wa mapato yaliyo kusanywa na serikali ya kitaifa baina ya serikali ya kitaifa na za kaunti; na baina ya serikali za kaunti.

Tangu kuanza kwa mwaka wa fedha Julai 2020, kumekuweko na mjadala mkali juu ya ugavi wa mapato ya kusambazwa kwa serikali za kaunti. Kizingiti kilicho katika Bunge la Seneti ambalo limewajibishwa, kupitia azimio, kuamua msingi wa kugawanya baina ya kaunti mgao wa mapato ya kitaifa ambayo hutengwa kila mwaka kwa ngazi ya serikali za kaunti. CRA iliunda mbinu mpya ya kugawanya mapato kwa msingi wa majukumu, idadi ya watu na viwango vya umasikini. Hapo awali, idadi ya watu, umasikini na ukubwa wa eneo vilikuwa ndio kichocheo cha ugavi wa mapato. Lakini, katika mbinu iliyofanyiwa marekebisho, kaunti zilizo na idadi kubwa ya watu lakini eneo dogo zitapata pesa zaidi kuliko zile zilizo na idadi ndogo ya watu lakini eneo kubwa.

Mvutano uliopo sasa ulioshuhudiwa kwa wanasiasa wote na mashirikiano nchini Kenya juu ya ugavi wa mapato kwa kaunti 47 umedhihirisha sura halisi ya udhalimu wa idadi katika nchi za kidemokrasia. Walo wengi ndio ufunguo wa kudumisha mamlaka ya kisiasa katika demokrasia, na hivyo basi kupata hisa ya windo la simba katika ile inayoitwa keki ya kitaifa (ugavi wa mapato). Huku kaunti zilizo dhaifu Kidemokrasia zenye idadi ndogo ya wakaazi zikicheza dori kwa kujaribu kusukuma ugavi adilifu wa mapato wenye kuakisi maendeleo sawa na ya kudumu katika utoaji huduma pamoja na uwekezaji wa rasilimali, juhudi hii ni mithili ya kukata kiu kwa kufukuzia mangati.

Huku siasa za 2022 zikizingua, ni wazi kwamba mpango wa mbinu ya kuzigawanya Sh316.5 bilioni ($31 milioni) umevurugwa na wanasiasa ili kutumikia matarajio yao ya kisiasa. Siasa za ubinafsi zilizoundwa na mfumo fisidifu wa kirasilimali huyatanguliza maslahi ya mtu binafsi juu ya raia wa kawaida. Hili linaelezea wazi kuwa ugavi wa mapato ni chombo cha kufikia malengo ya kisiasa na sio kuwanufaisha umma kama inavyo dhaniwa. Fauka ya hayo, ugavi wa mapato chini ya serikali za kirasilimali hutia vikwazo zaidi vya kiuchumi na kifedha kupitia kutoza kodi vikimu maisha (bidhaa na huduma).




Ukusanyaji na ugavi wa mapato ya dola chini ya Khilafah huunda mazingira

mwanana kwa raia kufikia ustawi wa kiuchumi. Katika Uislamu, imeharamishwa utozaji kodi vikimu maisha kwani hili husababisha kuenea kwa umasikini. Ama ukusanyaji wa mapato na ugavi wake, haya yameainishwa waziwazi na Shariah ambayo imeonyesha mipaka wazi baina ya mali ya dola, mali ya umma na mali ya kibinafsi. Hakuna nafasi kwa kampuni za kibinafsi kumiliki kipekee manufaa kutoka kwa rasilimali za umma kama








inavyo onekana katika uchumi wa kirasilimali, kwani Uislamu umefafanua maumbile ya mali za umma na ugavi wa mapato yake yaliyozalishwa na hivyo basi kuunda uchumi madhubuti na wenye nguvu.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Office of Hizb ut Tahrir na**
**Ali Omar**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**




////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////

# PENSHENI KWA WABUNGE WA ZAMANI: MPANGO WA KUWAKANDAMIZA WANYONGE

Mnamo Alhamisi, 6 Agosti 2020, Bunge la Kitaifa la Kenya lilipitisha Mswada wa 2019 wa Mabadiliko ya Pensheni ya Bunge, ambao kwamba lau Rais ataweka saini utakuwa sheria na kuifanya serikali kuwalipa wabunge wa zamani kitita cha takribani bilioni Sh1.15 kama pensheni ya ziada (Daily Nation, Alhamisi, 06/08/2020).

Maamuzi hayo yanalenga kumakinisha hali iliyoko na kuipa kipaombele badala ya masuala muhimu yanayowakabili Wakenya ambao wanataabika katika maisha yao kutokana na sababu zifuatazo:

**Kwanza,** janga la Covid-19 limevunjilia mbali uti wao wa kijamii na kiuchumi kiasi kwamba biashara nyingi zinafungwa na ilhali nyingine ziko katika mchakato wa kuwaachisha kazi baadhi ya wafanyakazi wao ili kukabiliana na athari za janga hilo la kiulimwengu. Kwa kuongezea, serikali inapatiliza janga hilo ili kuvuna manufaa ya kifedha kutoka kwa taasisi za kifedha na wale wanaoitwa washirika wa kimaendeleo kwa kuchukua mikopo mipya na kutafuta misaada ya kifedha kwa kisingizio cha kupambana na maradhi.

**Pili,** kuzidi kwa deni la umma ambalo limekuwa kutoka trilioni Sh5.7 mnamo 2019 hadi trilioni Sh6.65 kufikia Mei 2020! Imeifanya hali ya deni ya Kenya kuwa suala la kutia wasiwasi na kulazimisha mashirika ya kimataifa kutathmini upya hali ya kutamausha ya deni la Kenya na kuitoa katika kiwango cha chini hadi juu na mustakbali unaendelea kuwa mbaya (The Star, Jumatatu, 20/07/2020). Madeni yanaongezeka kutokana na hamu ya serikali kubuni miradi ghushi mikubwa ili kuwahadaa raia kuwa kukamilika kwake itabadilisha hali zao za maisha; lakini badala yake sio chochote bali ni njia za kufuja fedha na kuendeleza ufisadi! Mambo yatazidi kuwa mabaya kwani Baraza liliidhinisha mnamo Machi 2020, Sera ya Deni la Ummah na Kukopa ya 2020 ili kuziwezesha serikali za kaunti kukopa (The Star, Jumatatu, 27/07/2020).

**Tatu,** sekta ya elimu imekwama huku wazazi hawajui mustakbali wa watoto wao kwani kalenda ya masomo ya 2020 imefutiliwa mbali kwa ukamilifu. Uwekezaji wa kifedha na kiakili wote umepotea. Yote haya ikiwa ni natija ya kukosekana fedha za kutosha kuweza kukidhi gharama za ujenzi wa miundo mbinu inayotimiza masharti ya usalama kwa mujibu wa Covid-19.

**Nne**, kuzidi kwa mikakati ya ushuru inayowapatliza watu ambayo inatozwa na serikali ambayo ina hakikisha kuwa inakazanisha kitanzi cha kiuchumi katika shingo za raia kwa kuwatoza asilimia 3 za ushuru wa uzalendo kwa wafanyi biashara wadogo na asilimia 15 za ushuru wa makadirio. Na kuyapelekea maisha kuwa magumu zaidi kwa raia wengi ambao wanaishi kwa njia ya mkono kuelekea kinywani maishani mwao!

**Table 10: Indicators of Total Government Debt**

| | Jun-18 | Jun-19 | Sep-19 | Dec-19 | Jan-20 | Feb-20 | Mar-20 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Domestic debt (KSh Billion) | 2,478.84 | 2,785.94 | 2,851.64 | 2,942.10 | 3,003.70 | 3,040.96 | 3,071.85 |
| Public & Publicly Guaranteed External debt (US $ Billion) | 25.34 | 29.55 | 29.95 | 30.66 | 30.95 | 30.87 | 30.69 |
| Public & Publicly Guaranteed External debt (KSh Billion) | 2,560.20 | 3,023.14 | 3,111.80 | 3,106.82 | 3,112.90 | 3,117.04 | 3,212.63 |
| **Total public debt (KSh Billion)** | **5,039.03** | **5,809.08** | **5,963.44** | **6,048.93** | **6,116.60** | **6,158.00** | **6,284.49** |

Source: National Treasury and Central Bank of Kenya

Sababu hizo hapo juu ni sehemu tu ya

sababu nyingi ambazo zinafichua kwamba tawala za kisekula za kirasilimali hazisimami juu ya msingi wa kulinda na kusimamia mambo ya watu katika hali ya ubinadamu. Badala yake zipo kuwahudumikia wachache waliojibandika kuwa ndio viongozi na ambao wanafanya bidii kudumisha hali iliyoko kwa kujizawadi na kujilinda kutokamana na moto wa kiuchumi kwa kutumia migongo dhaifu ya mashini za kupiga kura “raia”! Kwani tawala hizi zipo kuhakikisha tu zinafikia maslahi na manufaa yao ya kilafi.

Kinyume chake ni kuwa ndani ya nidhamu ya uongozi ya Khilafah inayoongozwa na kiongozi mchamungu, Khalifah ni msimamizi wa raia wote Waislamu na wasiokuwa Waislamu katika hali ambayo anafahamu jukumu alilopewa na Mwenyezi Mungu (swt) na haki walizopewa raia na Mwenyezi Mungu (swt). Khalifah ni mchungaji wa raia na atahesabiwa Siku ya Kiyama kuhusu hilo.

**عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ أَلَا كُلُّكُمْ رَاعٍ وَكُلُّكُمْ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ فَالْإِمَامُ الَّذِي عَلَى النَّاسِ رَاعٍ وَهُوَ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ...**

Abdullah ibn Umar ameripoti: Nabii wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake, alisema, **“Kila mmoja wenu ni mchungaji na atahesabiwa kwa uchunga wake. Kiongozi (Khalifah) wa watu ni mlinzi na atahesabiwa kwa anaowatawala…”** Uislamu unadhamini mtu binafsi katika raia wa Khilah mahitaji yake msingi; chakula, mavazi na makaazi; na Khilafah itafanya bidi kuhakikisha inatoa mahitaji ya jamii; afya na elimu miongoni mwa mengine na wakati huo huo kutoa nafasi ili kukidhi mahitaji ya ziada.

Katika nidhamu ya Khilafah hakuna aliye juu y sheria na kila mmoja anatakiwa kutendewa kwa mujibu wa maelekezo ya Shari’ah ya Kiislamu pasina kuzingatia ima yuko uongozini au la, rangi, kabila au cheo. Hivyo basi, upendeleo na unyanyapaa wa aina yoyote hautoruhusiwa kattu! Hivyo basi tufanyeni kazi usiku na mchana kwa ushirikiano kuondosha hali iliyoko duniani na kuleta hali mpya chini ya uongozi wa uadilifu, Khilafah.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**


MPS, STOP BITING THE HAND THAT FEEDS YOU
MPs WAACHE MPANGO YA KANDO



//////////////////////////////////////////////////////////////////////////////

# MAKUBALIANO YA IMARATI NA MAYAHUDI .. KHIYANA JUU YA MSITARI WA UNAFIKI UNAOONEKANA

Katika taarifa ya pamoja mnamo 13 Agosti 2020, Imarati, Amerika na umbile la Kiyahudi zilitangaza makubaliano baina ya Raisi wa Amerika Donald Trump, Waziri Mkuu wa umbile la Kiyahudi Netanyahu, na Mfalme Mtarajiwa wa Abu Dhabi Mohammed bin Zayed ya kufanya mahusiano kamili ya pande mbili kati ya umbile la Kiyahudi na Imarati. Mwenyezi Mungu Mtukufu asema kuhusu haya:

**(يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ لاَ تَتَّخِذُواْ الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى أَوْلِيَاء بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاء بَعْضٍ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللّهَ لاَ يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ * فَتَرَى الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ يُسَارِعُونَ فِيهِمْ يَقُولُونَ نَخْشَى أَن تُصِيبَنَا دَائِرَةٌ فَعَسَى اللّهُ أَن يَأْتِيَ بِالْفَتْحِ أَوْ أَمْرٍ مِّنْ عِندِهِ فَيُصْبِحُواْ عَلَى مَا أَسَرُّواْ فِي أَنْفُسِهِمْ نَادِمِينَ)**

**"Enyi mlio amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu. Utawaona wale wenye maradhi nyoyoni mwao wanakimbilia kwao wakisema: Tunakhofu yasitusibu mabadiliko. Huenda Mwenyezi Mungu akaleta ushindi au jambo jingine litokalo kwake wakawa wenye**

**kujuta kwa waliyo yaficha katika nafsi zao."** [Al-Ma'ida: 51-52].




Ummah wa Kiislamu haukushangazwa na khiyana hii iliyo tangazwa na Imarati, na vipi utashangazwa wakati ambapo umeonja kutoka kwa watawala hawa vibaraka Ruwaibidha, aina kadha wa kadha za khiyana, uhaini, utovu wa dini na ukosefu wa ari, mengi mno kiasi cha kukadiriwa na makumi ya vizazi?! Hakika, watawala wa Dola za Ghuba, hususan, wamefanya kila juhudi katika miaka ya hivi karibuni kuufanya ulimwengu ujue nia yao ya kuufuata mpango wa Amerika wa kusawazisha mahusiano na umbile la Kiyahudi. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

(وَمِنَ الْأَعْرَابِ مَن يَتَّخِذُ مَا يُنفِقُ مَغْرَماً وَيَتَرَبَّصُ بِكُمُ الدَّوَائِرَ عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوْءِ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ)

**"Na katika Mabedui hao wapo wanao fikiri kuwa wanayo yatoa ni gharama ya bure, na wanakungojeleeni mambo yakugeukieni. Mageuko maovu yatakuwa juu yao! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua."** [At-Tawba: 98].

Ujasiri huu uliolaaniwa juu ya Ardhi Iliyo Barikiwa (Palestina) unaweza tu kukomeshwa na Ummah wa Kiislamu kupitia hatua uliochukua katika kuukomboa Msikiti wa Al-Aqsa kutokana na uchafu wa Makruseda, ni hatua hiyo hiyo ndio Ummah unasifia ushujaa wake, na ni hatua hiyo hiyo ambayo kwayo Ummah unaendelea kuwapa watoto wao majina ya Umar, Khalid na Salahuddin… Kila wakati Ummah wa Kiislamu ulipotaka kuikomboa Bait ul-Maqdis (Jesrusalem), uliiendea na majeshi ya Khilafah. Lakini yako wapi majeshi ya Khilafah leo?

**Enyi Waislamu:**

Tunajua kwamba namna Wamagharibi watakavyourudia "Mchezo: Mtawala wa Kiislamu anayetangaza kuiteka kwake Palestina", imani yenu kuwa umbile la Kiyahudi linakaribia kutoweka mikononi mwa Ummah wa Kiislamu haitabadilika. Bali, tunajua kwamba msimamo wenu halisi ni ule ambao Khalifah Abdul Hamid, Mwenyezi Mungu amrehemu, aliandika kwa kusema: "…maadamu niko hai, mkono wangu kukatwa na kiwembe sio uchungu zaidi ya kushuhudia Palestina ikitenganishwa kutoka katika dola ya Khilafah na hili halitatokea."

**Hapa tunalirudia swali: Yako wapi majeshi ya Khilafah leo?!**

**Jibu lake ni kuwa majeshi ya Khilafah yatazali**




**wa mara tu baada ya tangazo la ahadi ya utiifu *(Bay'ah)* kwa Khalifah, hii ni kwa sababu Ba'yah huanzishwa pekee na wale wanaoweza kumpa Khalifah jeshi ambalo kwalo atalinda Dar al-Islam (Makaazi ya Uislamu) na kufungua nchi, kwa njia ambayo Maanswari walisema katika bay'ah ya pili ya Aqabah, ambapo dola ya kwanza ya Kiislamu ilisimamishwa.** Albara bin Ma'roor alimwambia Mtume (saw):

"والذي بعثك بالحق لنمنعك مما نمنع منه أزرنا، فبايعنا يا رسول الله، فنحن والله أهل الحرب"

**"Naapa kwa Yule aliyekutumiliza kwa haki, tutakulinda kama tunavyolinda watoto wetu, hivyo basi chukua ahadi yetu ya utiifu ewe Mtume wa Mwenyezi, Naap kwa Mwenyezi Mungu sisi ni watu wa vita."**



Hivyo basi, leo na wakati huu tunaamsha ari ya Uislamu katika watu wanaomiliki nguvu na uwezo, kufanya kazi na Hizb ut Tahrir ili kutoa Bay'ah kwa imam wa Waislamu "khalifah", ili pamoja naye, wakiondoe kisu kilicho kitwa mgongoni mwa Ummah wa Kiislamu, nacho ni watawala makhaini, kisha pamoja naye, wakiondoe kisu kilicho kitwa moyoni mwa Ummah wa Kiislamu, nacho ni umbile la Kiyahudi, mnyakuzi wa Ardhi Iliyo Barikiwa. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

(يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ)

**"Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu."** [Muhammad: 7].

**Mh. Salah Eddine Adada**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**




////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////////

# UISLAMU NA WAISLAMU WANASHAMBULIWA KWA KISINGIZIO CHA KUPAMBANA NA UGAIDI: IKO WAPI NGAO NA MLINZI WA UISLAMU NA WAISLAMU?

Mnamo Jumapili, 16 Agosti 2020, Waislamu nchini Kenya kwa mara nyingine waliamkia taarifa za kutekwa nyara kwa Sheikh Khalid Swaleh, Ustadh Juma Shamte na Hassan wote kutoka Markaz Noor iliyoko Mtondia, Kaunti ya Kilifi. Watekaji nyara wanadaiwa kuwa ni maafisa kutoka Kitengo cha Kupambana na Ugaidi (ATPU) ambao walivamia majengo hayo mwendo wa saa 7 usiku (Daily Nation, 16/08/2020). Tukio hili linakuja miezi 3 tu baada ya tukio jingine la kinyama ambalo lililotokea mnamo Jumamosi, 30 Mei 2020 eneo la Kibundani, Kaunti ya Kwale ambapo Waislamu waliamkia habari za kuuliwa kwa Muislamu mwanamume, Mohamed Rahma Mapenzi (miaka 41) watoto wake wawili, Swalia Rahma (miaka 6) na Idd Rahma (miaka 3). Kwa kuongezea wanachama wa familia yake iliyobakia walijeruhiwa vibaya mno huku mkewe aliyekuwa na mimba ya miezi minane, Mwanahalima Mwachili alipoteza mimba yake wakati alipopelekwa hospitali ya Msambweni akiwa katika hali mbaya kwa kupigwa risasi tumboni na mguuni (The Standard, 31/05/2020). Ni jukumu letu kushughulishwa na yale ambayo yanawafika kaka na dada zetu Waislamu kwani Mwenyezi Mungu (swt)

asema: إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ "Hakika Waumini ni ndugu" (Al-Hujurat: 49: 10) na Mtume (saw) alisema: لا يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ حَتَّى يُحِبَّ لأَخِيهِ مَا يُحِبُّ لِنَفْسِهِ "Hakuna mmoja wenu atakayekuwa na imani mpaka pale atakapomtakia ndugu yake (Muislamu) yale anayojitakia yeye" (Sahih al-Bukhari).

Matukio hayo hapo juu ni sehemu tu ya matukio ya ukandamizaji ambayo Waislamu wanakabiliwa nayo nchini Kenya na duniani kote kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi na misimamo mikali. Vitendo hivyo hapo juu vinafichua yafuatayo:




Kwanza, Uislamu na Waislamu ndio kafara katika vita dhidi ya ugaidi na misimamo mikali nchini Kenya na kwingineko. Kwa kuwa asasi za kiusalama zinapotumia 'kibali' cha ugaidi basi hatima yako huwa imekwisha na ule unaoitwa msingi wa huna hatia mpaka itakapothibitishwa kuwa una hatia chini ya nidhamu yenye uwezo ya mahakama ambayo haiendeshwi na ushawishi wa serikali na Wamagharibi ni uongo wa wazi!

Pili, Uislamu na Waislamu wanakabiliwa na njama za kudumu kutoka kila kona ya ulimwengu za maadui wa Uislamu na Waislamu ambao wanakwenda mbio kutumia rasilimali zao zote ili kuhakikisha kuwa nuru ya Uislamu haipenyi na kutawala ulimwengu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii katika ngazi ya kimfumo. Lakini, Mwenyezi Mungu (swt) asema: وَيَمۡكُرُونَ وَيَمۡكُرُ ٱللَّهُۖ وَٱللَّهُ خَيۡرُ ٱلۡمَٰكِرِينَ "Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango." (Al-Anfal 8:30).

Tatu, Uislamu na Waislamu wanakabiliwa na mashambulizi ya kijamii kutoka kwa nidhamu ya kihuria inayolazimishwa juu yao na mfumo wa kisekula wa kirasilimali ambao unakwenda mbio kuhakikisha kuwa Waislamu wanabeba ufahamu wa tupo ndani 'Uislamu Poa' ambao umejengwa kuhakikisha kuwa Waislamu wanatafuta muongozo kutoka kwa Washington, London na Ufaransa n.k. Hatima yake ni kuishilia kuwa utambulisho wa kisekula lakini wamebakia na majina ya Kiislamu.

Nne, Uislamu na Waislamu wanakabiliwa na njama ovu za kiuchumi kiasi kwamba

Muislamu yeyote ambaye anajitolea na kujifunga na vitendo vya kutoa msaada anabandikizwa kuwa ni 'mdhamini wa ugaidi na misimo mikali.' Hivyo basi anaangamizwa kiuchumi na kuwapelekea Waislamu wengi wakitaabika kimya kimya kutokana na kuwashuhudia kaka na dada zao wakiangamia kwa shida za kiuchumi pasi na msaada wowote kutoka kwa tawala za kisekula za kirasilimali za kilafi.

Tano, wale wanaoitwa walinzi na watetezi wa haki za kibinadamu na utiifu kwa sheria hawaonekani pale Uislamu na Waislamu wanapokabiliwa na mashambulizi. Lakini, pale wanapoamua kujitokeza huja tu kwa ajili ya lengo la kuuza sura na kupatiliza hisia na kuvuna msaada wa kifedha kutoka kwa watu kwa kuwahadaa kuwa wanafanyiakazi ajenda ambayo ina sura mbili iliyosimama kwa msingi kuwa 'Magaidi na Wenye Misimo Mikali' hawana haki kwani ni tishio kwa wanadamu.

Sita, wale wanaoitwa watawala na viongozi Waislamu hapa nchini na kimataifa sio chochote bali ni kiunganishi cha asasi za serikali ambao wameuza roho zao kwa shetani na hivyo wanapiga njama dhidi ya Uislamu na Waislamu na kupanga mipango pamoja na maadui. Hivyo basi, wao ndio wanaosimamia mauaji  maovu yanayofanyiwa Waislamu kwa kutunga sheria za kupambana na ugaidi na misimamo mikali.

Orodha ni ndefu kuanzia Pakistan, Somalia, Saudi Arabia, Yemen, Jordan, Misri, Uzbekistan, Tunisia, Urusi, Uchina (Xinjiang), Afghanistan na mataifa mengine.




Saba, Uislamu na Waislamu wamesongeka, hawana nafasi ya kupumua kutokana na uchungu na wako njia panda baada ya kujaribu kila njia za kibinadamu na kufeli. Baadhi yake zikijumuisha kushiriki katika chaguzi za kidemokrasia wakitarajia kuboresha hali zao kwa kuwachagua wasanii wa kisiasa wanaotumia hisia za Kiislamu ili kuingia madarakani lakini hawatimizi kitu. Bali hugeuka na kuwa ndio watekelezaji madhalimu wa ukandamizaji wa Waislamu katika kila nyanja ya maisha kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hivyo basi, kila mzunguko mpya wa uchaguzi matumaini yao hupungua! Wanabakia na swali; ni ipi njia ya kujitoa katika


mateso haya ya kinidhamu wanayotendewa?

Jibu msingi la swali hilo hapo juu si jingine isipokuwa ni kuitikia ulinganizi wa mabadiliko ya kimfumo kwa msingi wa Shari’ah ya Kiislamu ambayo vyanzo vyake ni: Qur’an, Sunnah, Ijma’ Sahaba na Qiyas. Kwani tupo katika hali hii ya shida kwa sababu ya kwenda kinyume na Shari’ah ya Uislamu kwa kutoitekeleza. Mwenyezi Mungu (swt) asema: وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِى فَإِنَّ لَهُۥ مَعِيشَةً ضَنكًا وَنَحْشُرُهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَـٰمَةِ أَعْمَىٰ “Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu” (TaHa 20: 124). Badala yake tumekumbatia katiba na sheria zilizotungwa na wanadamu ili kusimamia maisha yetu. Tumemchagua mwanadamu kututungia sheria/kutuhukumu badala ya Mwenyezi Mungu (swt) anayesema: وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ ٱللَّهِ حُكْمًا “Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu” (Al-Ma’idah 5: 50), إِنِ ٱلْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ “Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu” (Al-An’am 6: 57), إِنِ ٱلْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ “Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu” (Yusuf 12: 40). Ni lazima tufahamu na tuamini yale ambayo Mwenyezi Mungu (swt) anayoyasema: إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلْإِسْلَـٰمُ “Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu” (Aal-Imran: 19). Kukatikiwa kwetu lazima tuitikie mwito wa Mwenyezi Mungu (swt): يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱدْخُلُوا۟ فِى ٱلسِّلْمِ كَآفَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا۟ خُطُوَٰتِ ٱلشَّيْطَـٰنِ ۚ إِنَّهُۥ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ “Enyi mlio amini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu, wala msifuate nyayo za Shetani; hakika yeye kwenu ni adui aliye wazi” (Al Baqarah 2: 208).




Njia pekee ya kutoka katika maangamivu ipo katika kujiunga na juhudi za Hizb ut Tahrir na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya kusimamisha Dola ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume. Khilafah chini ya kiongozi mukhlis, Khalifah, itakuwa ndio ngao na mlinzi madhubuti wa Uislamu, Waislamu na raia wasiokuwa Waislamu popote walipo pasi na kuzingatia rangi, cheo au kabila. Imesimuliwa kutoka kwa Abu Huraira kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alisema: إِنَّمَا الإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيُتَّقَى بِهِ “Imam (Khalifah) ni ngao kwao (Waislamu). Nyuma yake wanapigana na wanajilinda (kutokana na madhalimu na wakandamizaji)”

(Muslim). Pia ni dhambi kubwa kutofanyakazi ya kusimamisha Khilafah. Mtume (saw) alisema: وَمَنۡ أَعۡرَضَ عَن ذِكۡرِي فَإِنَّ لَهُۥ مَعِيشَةٗ ضَنكٗا وَنَحۡشُرُهُۥ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ أَعۡمَىٰ "Yeyote anayeondosha mkono wake kutoka katika utiifu (wa Khalifah) atakutana na Mwenyezi Mungu ilhali hana ushahidi juu yake, na yeyote anayekufa pasi na ahadi ya utiifu (kwa Khalifah) juu ya shingo yake anakufa kifo cha kijahiliyya" (Muslim).




Ni mfumo wa Kiislamu chini ya Khilafah iliyosimama kwa njia ya Utume ndio pekee inayodhamini utulivu, hadhi na heshima sio tu kwa Waislamu bali kwa wanadamu wote duniani ambao wanataabika kutokana na majanga ya kila siku yanayoendelezwa na wakoloni Wamagharibi wakiongozwa na Amerika na washirika wake. Hakuna mbadala isipokuwa #TurudisheKhilafah ambayo ndio hitajio la wakati huu na matumaini pekee kwa Uislamu, Waislamu na wanadamu wote baada ya kumaliza njia zote ambazo haziingii akilini kuanzia mashariki na magharibi na kaskazini hadi kusini.

Wakati ni sasa kuwekeza juhudi pale palipo na malipo ya hapa duniani kwa muda mfupi na akhera ya milele. Hakuna kupoteza nguvu katika yale ambayo yanamkasirisha Mwenyezi Mungu (swt) kama vile kujiunga na vyama vya vya kisiasa vya kisekula vya kirasilimali ambavyo vinalingania suluhisho za kidemokrasia ambao wanaopigia debe na washindi ni vibaraka wa mabwana wakoloni. Bali, jiunge na uwe sehemu ya chama cha Kiislamu cha Hizb ut Tahrir kilichobuniwa kwa msingi wa mfumo wa Kiislamu ambacho macho yake yako makini kuleta mabadiliko ya kimfumo duniani kwa njia ya Uislamu kwa kurudisha maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha Khilafah ambayo ni ngao, mlinzi na mama wa faradhi zote za Kiislamu. Mwenyezi Mungu (swt) asema: بِنَصۡرِ ٱللَّهِۚ يَنصُرُ مَن يَشَآءُۖ وَهُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلرَّحِيمُ*وَعۡدَ ٱللَّهِۖ لَا يُخۡلِفُ ٱللَّهُ وَعۡدَهُۥ وَلَٰكِنَّ أَكۡثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعۡلَمُونَ "Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Na ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu. Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake. Lakini watu wengi hawajui" (Ar-Rum 30: 5 – 6).

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**


Khilafah is the shield of Muslims.
Open massacre of Muslims, surge to actio Muslim arme forces.
THEN WHAT ?

# Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari

## Uzinduzi Rasmi wa Kampeni ya Hizb ut Tahrir / Kenya Chini ya Kauli Mbiu 'Kila Mmoja Wenu ni Mchungaji'

Janga la maambukizi ya virusi vya Korona linaendelea kuchua maisha ya watu wengi ulimwenguni pia limepelekea kusitishwa kwa amali nyingi za kiuchumi; na kuharibu njia za watu za kujikimu kimaisha. Pia limepelekea kufungwa kwa taasisi za masomo ambapo imesababisha janga jengine nchini Kenya; ongezeko la mimba za wasichana wa shule. Data kuhusu mimba za matineja iliyotolewa hivi majuzi inaonyesha takriban wasichana wa shule 152,820 kote nchini wamepachikwa mimba tangu kufungwa kwa shule. Ingawa serikali imepuuzilia mbali tarakimu hizo ikizitaja kama za kuchukiza, ukweli bado ungalipo kuwa vitendo vya ngono ni miongoni mwa maovu yaliyokithiri ndani ya jamii ya kisekula.

Kwa wasiwasi mkubwa, Hizb ut Tahrir / Kenya inazindua kampeni kubwa chini ya mada**: "Kila Mmoja Wetu ni Mchungaji"** kuanzia tarehe 25 Agosti 2020 hadi 31 Disemba 2020.

Msururu wa matukio wakati wa kampeni hii utajumuisha darsa za ummah misikitini, jaula mitaani na midahalo ya moja kwa moja, miongoni mwa mengine. Mada kuu ya mazungumzo itakuwa ni namna gani Urasilimali na itikadi yake potofu ya usekula zimechangia sio tu janga la kijamii bali majanga yote katika kila nyanja ya maisha. Ummah unaojumuisha wazazi na walezi watakumbushwa kuhusu jukumu lao la kuwalinda watoto wao kutokana na uvamizi wa thaqafa ya Kimagharibi kupitia kuhakikisha kuwa wanaasisi Kitambulisho cha Kiislamu katika watoto wao.

Tunausihi ummah kujiunga nasi katika kampeni hii kwani ni sehemu ya kazi tukufu ya kuamrisha mema (Maa'ruf) na kukataza maovu (Munkar).

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

Fuatilia alama ishara za kampeni**:**

**#Covid-19_Inafichua_Urasilimali**
**#Covid-19_Usekula_Unatenganisha_Dini**
**#Covid-19_ Majanga_ya_Umma_yaliogeuzwa rasilimali_na_Warasilima**


KORONA: KILA MMOJA WETU NI MCHUNGAJI

# Jarida la

# UQAB

